



AZIMIO NA. 5/2018

AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA TAKWIMU WA AFRIKA (*THE AFRICAN CHARTER ON STATISTICS*)

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Nchi za Umoja wa Afrika (AU);

KWA KUWA, Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, katika Mkutano uliofanyika, tarehe 4 Februari, 2009 waliazimia kuwa na Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*) kwa lengo la kuweka Mfumo wa kuratibu upatikanaji na usambazaji wa takwimu bora za kiuchumi, kijamii na mazingira zitakazotumika katika kupanga na kutolea maamuzi mbalimbali ya kiseru katika ngazi ya Taifa, Kanda na bara zima la Afrika;

KWA KUWA, hadi Mwezi Juni, 2017 nchi 22 (asilimia 69) kati ya Nchi 32 zilizosaini zilikuwa zimeridhia Mkataba huo ambao ulianza kutumika rasmi tarehe 8 Februari, 2015;

KWA KUWA, Tanzania ni mojawapo ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika iliyosaini Mkataba huo tarehe 23 Machi, 2012 lakini ni miongoni mwa nchi ambazo hazijaridhia Mkataba huu;

KWA KUWA, Mkataba huu kupitia Ibara ya 14 na 15 unabainisha kwamba, Nchi Wanachama zinapaswa kuridhia Mkataba huu ili

kupata nguvu za kisheria na kwamba baada ya nchi wanachama kusaini, unapaswa kuridhiwa kwa mujibu wa katiba za Nchi husika na kuanza kutumika siku thelathini (30) baada ya kuridhiwa na Nchi kumi na tano (15);

NA KWA KUWA, Tanzania kwa kuridhia Mkataba huu itafaidika na mambo yafuatayo:

- (a) kuwa na ulinganifu ulio bora zaidi wa viashiria vya kiuchumi na kijamii baina ya nchi za Afrika. Hii ni kutokana na kuwepo kwa mfumo imara wa uzalishaji takwimu rasmi zinazokidhi viwango vinavyokubalika katika Mfumo wa Takwimu wa Afrika (Africa Statistical System);
- (b) kuongezeka kwa ubora wa takwimu rasmi za Serikali na hatimae kuongezeka kwa matumizi ya takwimu hizo kitaifa na kimataifa hali ambayo itachochea uwekezaji wa ndani na nje ya nchi na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi, kupunguza umaskini, kuongezeka kwa mapato ya Serikali na ajira;
- (c) watakwimu nchini kuendelea kujengewa uwezo zaidi wa mbinu za kisasa za matumizi ya teknolojia kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa takwimu rasmi zitakazohitajika katika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa, Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals-SDG's*) ya mwaka 2030 na Agenda ya Afrika ya Mwaka 2063 kwa kutumia

ushirikiano uliopo miongoni mwa Nchi Wanachama wa Afrika (*South South Cooperation*);

- (d) kuendelea kufaidika na misaada ya kibajeti na kitaalam katika kuboresha nakuimarisha tasnia ya takwimu itakayotolewa kwa Bara la Afrika na wadau mbalimbali wakiwemo wa maendeleo, sekta binafsi na wengine ikijumuisha misaada nafuu ya kuboresha mifumo ya takwimu katika ngazi mbalimbali za utawala hapa Nchini.

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Mkataba huu na pia umuhimu wake kwa maendeleo ya Taifa, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Tatu, na kwa mujibu wa Ibara ya 64(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, linaazimia kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika uitwao "*The African Charter on Statistics.*" Bila kulazimika kutoa taarifa za takwimu ambazo zitaathiri maslahi ya Taifa.

Limepitishwa na Bunge leo tarehe 15 Novemba, 2018

Stephen Kagaigai
KATIBU WA BUNGE